# Mpango wa Makazi Mapya kwa Wakimbizi Waliodhaminiwa na Serikali ya Kanada



SWAHILI

GAR GAR GAR GAR GAR GAR

## Tangazo rasmi

Unavutiwa na kukaa nchini Kanada na maombi yako yameshapitiwa kwa mara ya kwanza na maafisa wa Kanada Na kwa sasa unasubiri na kujiuliza ni jambo gani litakalofuatia baadaye. Tangazo hili linatoa mwelekeo kuhusu hatua zitakazofuata katika utaratibu huu na kukuwezesha kujua mengi zaidi kuhusu nchi ya Kanada.



Citizenship and Immigration Canada
Citoyenneté et Immigration Canada

Canada

# Kile unachohitaji kujua kuhusu utaratibu wa makazi mapya

Uteuzi wako kama mkimbizi anayestahili (ukijumuisha mahojiano yako pale ambapo itahitajika) ni hatua muhimu katika hatua za makazi mapya, lakini si hatua ya mwisho.

Ikiwa umechaguliwa katika mpango huo wa makazi mapya kama mkimbizi aliyedhaminiwa na serikali [government-assisted *refugee* (GAR)], inaweza kukuchukuwa hadi miezi sita au zaidi kabla hujasafiri kwenda Kanada.

Haya ndio yatakayo tokea:

**Hatua za maombi**

- Kabla maombi yako hayajakubaliwa, wewe na familia yako lazima mfanyiwe uchunguzi wa kiafya. Lazima pia mchunguzwe kiusalama ili kuhakikisha kwamba hamjawahi kuhusika na vitendo vya uhalifu na ya kwamba hamtahatarisha usalama nchini Kanada. Halafu mfanyakazi mmoja wa ngazi ya juu kutoka idara ya uhamiaji ya Kanada atatoa uamuzi ikiwa mnaweza kuingia na kuishi nchini humo.
- Inaweza kuchukua baadhi ya miezi baada ya Uteuzi wako kabla ya kuombwa kufanya uchunguzi wa kiafya.
- Wafanyakazi wanaohusika na utoaji wa viza ya Kanada watachunguza mara tena maombi yako ili waone ikiwa umefaulu uchunguzi wa kiafya, wa kiusalama, na wa uhalifu.
- Endapo hutafaulu uchunguzi wa kiafya, wa kiusalama, na wa uhalifu, basi huenda usikubaliwe kuingia au kukaa nchini Kanada.
- Viongozi husika kwa niaba ya serikali ya Kanada watawasiliana na Shirika la Uhamiaji la Kimataifa [*International Organization for Migration* (IOM)] au shirika lingine lililoajiriwa na Serikali ya Kanada na kukajulisha matukio kuhusu maombi yako hapo itakapothibitishwa kwamba umekubaliwa kuingia na kukaa nchini Kanada na ya kwamba upo tayari kusafiri.
- Shirika la IOM au shirika lingine watakuhudumia katika shuguli za usafiri kuelekea Kanada.
- Katika baadhi ya nchi zingine, utakakaribishwa kwenda kuhudhuria mafunzo kuhusu Kanada (Canadian Orientation Abroad – COA) ambayo yanatolewa kabla ya kuondoka. Programu hii ya mafunzo kuhusu Kanada (COA) kabla ya kuondoka inadhaminiwa na Idara ya Uraia na Uhamiaji Kanada na inaendeshwa ulimwenguni kwote na IOM. Mafunzo haya yanatolewa bure. Katika mafunzo haya utajifunza kuhusu Kanada na pia juu ya huduma za uloezi zinazopatika kwa wahamiaji baada ya kuwasili nchini Kanada.

**Kuondoka kwenda Kanada**

- Shirika la IOM au shirika lingine watakujulisha terehe utakayo safiri kwenda Kanada. Pia watakuandalia tiketi, watakupeleka kwenye uwanja wa ndege, watakusaidia kuingia kwenye ndege na watakuhudumia kwa njia nyingine yoyote ile hapo kwenye uwanja wa ndege, kama itahitajika.

- Kama huna pasipoti au nyaraka zingine halali za kusafiria, Serikali ya Kanada itakupa nyaraka zitakazo kuwezesha kusafiri nchi ya Kanada.
- Gharama za kwenda Kanada, zikiwemo zile za uchunguzi wa kiafya zitalipwa na mkopo utakaopewa na Serikali ya Kanada.
- Huu ni mkopo na kwa hiyo itakupasa urudishie Serikali ya Kanada jumla ya kiwango cha pesa utakazopewa. Mnamo siku 30 baada ya kufika Kanada, lazima uanze kulipa pesa za usafiri na za uchunguzi wa kiafya. Unaweza kulipa kwa awamu na utakuwa na muda wa mwaka mmoja hadi miaka sita kwa kumaliza kulipa pesa zote, yote hayo ni kulingana na kiwango cha mkopo huo.
- Utakuwa pia na nafasi ya kutafuta kazi na kufanya kazi nchini Kanada ili uweze kujisaidia wewe na familia yako.
- Mara tu utakapofaulu uchunguzi wote na hati zako za kusafiria zikiwa tayari, shirika la IOM au shirika lingine watakupeleka kwenye uwanja wa ndege, watakukusaidia kuingia kwenye ndege na watakusaidia kukabiliana na wafanyakazi wa idara ya uhamiaji hapo kwenye uwanja wa ndege.

## Ufikapo Kanada kama mkimbizi aliyedhaminiwa na serikali




Ukiwa mkimbizi aliyedhaminiwa na serikali inamaanisha kwamba ufikapo Kanada, Serikali ya Kanada itakupa msaada wa kifedha ili uweze kujitegemea wewe mwenyewe kwa muda wa miezi kumi na miwili. Serikali pia italipia huduma za matibabu utakazohitaji baada ya kufika nchini humo.

- Wakati utakapofika nchini Kanada, wafanyakazi kutoka shirika linaloshughulikia huduma za uhamiaji watakukaribisha na kukushugulikia hapo kwenye uwanja wa ndege na watakusaidia mnamo siku chache za mwanzoni katika nchi yako mpya.
- Watakusaidia kupata mahala pa kukaa, kama vile nyumba ya wageni au hoteli. Hii ni makao ya muda mfupi na utakaa hapo mpaka pale utakapopata nyumba inayokufaa ambamo utaweza kukaa kwa muda unaotaka.
- Utapewa chakula na mavazi na utakutana na wahamiaji wengine wapya kama wewe.
- Wafanyakazi hawa kutoka shirika linaloshughulikia huduma za uhamiaji watajibu maswali yako na wataendelea kukusaidia kujiandaa katika maisha yako mapya nchini Kanada.

Mnamo wiki chache baada ya kufika, utaanza kupokea msaada wa kifedha kutoka Serikali ya Kanada. Hii itakusaidia kukidhi mahitaji yako kama vile ya chakula, samani, mavazi na mahitaji muhimu ya nyumbani. Utapewa pia posho kila mwezi kwa muda wa mwaka mmoja ili ujisaidie kwa chakula na mahala pa kuishi. Serikali pia italipia huduma za matibabu utakazohitaji baada ya kufika.

Zaidi ya hayo, watoaji huduma wataandaa mipango ya kukusaidia katika shughuli za kila siku, kama vile kutumia mfumo wa mabasi, kufanya miadi na daktari au benki. Mashirika haya yanaweza kukusaidia kujaza fomu, kupata kadi yako ya makazi, kuomba bima ya afya na namba ya jamii ya bima, n.k. Pia wanatoa huduma za ukalimani na tafsiri kusaidia mahitaji muhimu kama vile maelezo kuhusu afya yako hapo unapokutana na madaktari.

Watoaji huduma pia wanatoa huduma za mafunzo ya lugha ya Kiingereza au Kifaransa huku wakizingatia mahitaji yako. Itakuwa ni muhimu kwako kuendeleza na kuborehsa ujuzi wa lugha ili uweze kufanya kazi, kuzoea mazingira na kuwa mkaaji kamili katika jamii ya Kanada.

Hata ingawa Serikali ya Kanada itakupa msaada wa mwanzo kukusaidia kuanza maisha yako nchini Kanada, ni muhimu kwako kuwa na matarajio halisi. Kwa hiyo unapaswa kujiandaa kufanya kazi kwa bidii ili uweze kuishi vizuri nchini Kanada. Maisha yako ya baadaye nchini Kanada yatategemea sana juhudi zako.

## Makazi mapya na familia yako



Wakati wa hatua za uteuzi, wafanyakazi wa idara ya uhamiaji ya Kanada walikukumbusha kwamba wewe pamoja na mke wako na watoto wako mnaweza kuomba hifadhi kwa pamoja mkijaza fomu na hivyo kuweza kuja Kanada nyote pamoja. Kama kuna mabadiliko yoyote katika hadhi yako (kama vile uliolewa au kupata talaka) au kupata mtoto muda wowote kabla hujaja Kanada, lazima ulitaarifu Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia wakimbizi (UN refugee agency na Maafisa wa uhamiaji Kanada  ili majina ya watu hao wapya yaongezwe kwenye orodha ya familia yako.

Ni muhimu sana kuwaambia UNHCR na wafanyakazi wa Kanada kwamba mnataka kukaa kama familia. Lazima pia uorodheshe familia yako yote (ikiwa ni pamoja na watoto wako wote, kaka na dada, wazazi, mke au mume) bila kujali wanaishi na wewe au sehemu nyingine.

Ni muhimu uorodheshe watu wote wa familia yako hata kama hawataki kukaa Kanada kwa sasa.

Mtu yeyote ambaye hajaorodheshwa kwenye fomu yawezekana asikubaliwe kuja Kanada baadaye.

Kama una ndugu au marafiki wa karibu ambao tayari wamekwisha fika Kanada na ungependa kuishi karibu nao, lazima uwajulishe viongozi na wafanyakazi kwenye shirika la UNHCR na wale wa Kanada. Kadri iwezekanavyo, Serikali ya Kanada inajaribu kuwaweka wakimbizi katika jamii ambamo wataweza kupewa msaada na watu wanaowafahamu.

## Hadhi yako ya uhamiaji




Baada ya kuwasili nchini Canada, utapewa hati ikisema unaweza kuishi hapa kama mkazi wa kudumu. Hii ina maana kuwa ni halali kwako kukaa nchini Canada. Utaweza kufanya kazi au kwenda shuleni.

Kuna mahitaji maalum kuhusu muda gani lazima kuishi na kuwa katika nchi ya Canada kabla uweze kuomba uraia wa Canada. Mara baada ya kukidhi mahitaji yote, unaweza kuomba kuwa raia wa nchi ya Canada.


## Mahala pa kuishi nchini Kanada




Kanada ni nchi ya pili kwa ukubwa duniani yenye miji mingi mikubwa na miji midogo lakini pia kuna maeneo mengi makubwa yasiyokaliwa na watu. Miji mingi yapatikana katika maeneo ya kusini mwa nchi. Hii inawafanya watu kukaa mbali na watu wengine na inachukua muda mrefu kusafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine, hata kwa ndege. Kwa mfano, kati miji ya Toronto na Vancouver kuna umbali wa zaidi ya kilometa 4,300 au zaidi ya masaa manne kwa ndege. Unaweza kuhamia katika mji wowote ule unaoupenda.

Hata ingawa upo huru kuhamia sehemu nyingine nchini Kanada, tungekushauri ukae sehemu moja angalau kwa mwaka mmoja. Hii itakusaidia kunufaika na mipango ya huduma.

## Msaada nchini Kanada




Kuna vikundi vingi vya jamii na mashirikisho mengi kwa ajili ya wanaume, wanawake na watoto na unaweza kujiunga na mojawapo ya vikundi hivyo. Unaweza kujihusisha na shughuli za michezo kama mpira wa miguu au kuogelea, na kuna shughuli nyingi mnaweza kufanya kwa pamoja kama familia. Mnaweza kujiunga na baadhi ya vikundi bila malipo wakati ambapo itawabidi mlipe kiasi fulani cha pesa kwa kujiunga na vikundi vingine.

Kama kuna mkutano wa wageni katika eneo lako, jaribu kuhudhuria. Hii itakusaidia kupata marafiki kwenye jamii yako na kukusaidia kufahamu huduma zilizopo eneo lako.

Kukutana na watu katika jamii yako kunaweza pia kukusaidia kuishi vizuri nchini Kanada, kwa hiyo usiogope kuomba msaada kwa watu wengine.

## Maisha ya jamii nchini Kanada



Nchini Kanada, wanaume na wanawake ni sawa. Wana haki sawa na wanahudumiwa kwa kiwango sawa. Wanaume na wanawake kutoka jamii zote, tamaduni, rangi na dini mbalimbali wanashirikiana vizuri na wanapewa huduma kwa usawa.

Upo huru kutoa maoni yako nchini Kanada wakati huo huo ukiheshimu haki za wengine kufanya hivyo.

Huenda umezoea kuishi ukizungukwa na familia yako yote na huku wakikusaidia. Ufikapo Kanada, unaweza kuhisi upweke lakini haupo peke yako. Kama una jambo lolote, onana na mtu. Zungumza na mtu kutoka jamii yako. Kuna watu ambao wataweza kukusaidia kuishi vizuri nchini Kanada.

## Kudhamini familia yako




Mara ufikapo Kanada, unaweza kuwadhamini ndugu wengine ili wao pia waweze kuja Kanada. Hata hiyvo, unapaswa kujua kwamba hatua hii inaweza kuchukua muda mrefu, na huenda usiweze kuwaona ndugu zako kwa miaka mingi. Ndugu anachukuliwa kuwa ni mzazi, babu na bibi, mume/mke na watoto wanaokutegemea. Hakikisha ndugu hawa wanaorodheshwa kwenye maombi yako ya kuja Kanada. Kaka, dada, shangazi, wajomba, binamu na watoto wakubwa hawawezi kudhaminiwa baadaye.

Hakikisha watu wa familia yako wanajua kwa hakika mahala unakoishi nchini Kanada. Hakikisha wanafahamu anuani yako ikiwa ni pamoja na jina la mji na jimbo unaloishi.

## Kutafuta kazi







Japokuwa wewe na familia yako mtapata msaada wa kifedha mwaka wako wa kwanza nchini Kanada, ni wazo zuri kutafuta kazi ili uweze kujitegemea wewe na familia yako haraka iwezekanavyo. Kama unafahamu kuzungumza Kiingereza au Kifaransa, itakuwa rahisi kupata kazi.

Pia ni lazima ujue kama ukiwa na shahada, stashahada au cheti cha biashara, huenda visikubaliwe nchini Kanada. Itakuwa ni waajibu wa serikali ya jimbo unaloishi au baraza la sera katika mkoa wako kubainisha na kuhakikisha kuwa shahada yako au cheti chako au hati nyingine vinatambuliwa kisheria.

Pia unaweza kutaka kutuma pesa kwa ndugu na jamii waliobaki nyumbani huko katika nchi yako ya asili. Unaweza kufanya hivyo, lakini wakimbizi wengi huona ni vigumu kujisaidia wao wenyewe na waweze tena kupata pesa za ziada za kutuma nyumbani. Kumbuka, itachukua muda kuzoea mazingira mapya ya Kanada.

## Gharama za maisha

Utakapofika Kanada, utapewa msaada wa kifedha kutoka serikalini ya nchi hiyo kwa muda wa hadi miezi kumi na miwili (12).


Mara tu msaada huo utakapokwisha, basi litakuwa ni jukumu lako wewe mwenyewe kujigharimia mahitaji ya chakula, kodi ya nyumba, umeme, maji, nguo na ushuru. Ni muhimu kujifunza namna ya kutumia pesa zako.

## Kuhusu shule



Hutahitaji kulipa karo ya shule kwa ajili ya watoto wako wanaojiunga na shule la msingi au la upili (sekondari). Watoto wote kati ya miaka sita na miaka kumi na sita lazima waende shule. Hivyo ndivyo isemavyo sheria. Wanafunzi wengi wanahudhuria shule la sekondari mpaka wanapohitimu stashahada (kwenye miaka ya 18). Baada ya kumaliza sekondari, baadhi yayo waaweza kwenda chuo kikuu au chuo kidogo, kama wanaweza kulipia. Mtu yeyote anayetaka kusoma chuo kikuu ni lazima awe na pesa za kutosha.

## Kuhusu afya ya meno



Japokuwa serikali inatoa huduma za afya kama vile kuonana na daktari na kulipia huduma za dharura kwa ajili ya meno katika mwaka wako wa kwanza nchini Kanada, haijumuishi gharama za kawaida za matibabu ya meno. Ukienda kuonana na daktari wa meno, utakuwa na jukumu la kulipia gharama wewe mwenyewe.

## Chakula na maji



Nchini Kanada, maji ni safi kwa kunywa. Ndani ya kila nyumba kuna maji ya moto na maji ya baridi. Unaweza kupata maji wakati wowote, mchana kama vile usiku. Unachopaswa kufanya ni kufungua bomba la maji na kulifunga unapomaliza kutumia.

Watu wa tamaduni mbalimbali wanaishi nchini Kanada. Unaweza kupata vyakula vingi unavyokula kama vile mchele, mkate, mboga mboga, viungo, dengu na kuku kwenye duka lililopo karibu nawe. Nchini Kanada kunapatikana pia maduka mengine mengi yanayouza vyakula maalumu kama vile nyama ya mbuzi, ambayo mara nyingi haipatikani katika maduka ya kawaida. Chakula halali pia kinapatikana.

## Kuhusu Dini






Dini nyingi zinapatikana nchini Kanada. Unaruhusiwa kuabudu katika dini yako. Sheria ya Kanada inahitaji kila mtu aheshimu dini ya mwenzake. Hutaombwa wala kulazimishwa kubadili dini yako. Uhuru wa dini ni mojawapo ya haki za msingi katika nchi ya Kanada.

## Hali ya hewa

Kuna aina nne za hali ya hewa nchini Kanada: msimu wa kuchipuka (*Spring*), msimu wa kiangazi (*Summer*), msimu wa demani (*Autumn or fall*) na msimu wa barufa (*winter*). Kanada ni nchi kubwa sana na hali ya hewa inaweza kuwa tofauti katika sehemu mbalimbali nchini. Katika msimu wa kuchipuka (Machi, Aprili na Mei) ni wakati wa mvua sehemu nyingi nchini Kanada, na hali ya hewa inaweza kuwa baridi kidogo. Wakati wa kiangazi (Juni, Julai and Agosti), hali ya hewa ni joto sana katika sehemu nyingi nchini. Wakati wa mchana, hali ya joto mara nyingi ni juu ya nyuzi 20°C na wakati mwingine inaweza kupanda mpaka nyuzi 30°C. Wakati wa demani (Septemba, Oktoba na Novemba), hali ya hewa ni ya baridi na pia mvua inaweza kunyesha kwa wingi. Wakati wa barufa (Disemba, Januari na Februari), hali ya hewa sehemu kubwa ya nchi mara nyingi ni chini ya nyuzi 0° na inaweza kushuka mpaka chini ya nyuzi -30°, mchana hata usiku. Baridi inaweza kuwa kali sana na unapaswa kuvaa ikupasavyo.









## Ushauri wa mwisho

Kuanza maisha mapya nchini Kanada ni jambo la furaha ila baadhi ya watu huona kuwa ni jambo gumu. Inachukua muda kuzoea, kwa hiyo itabidi uwe mvumilivu. Wahamiaji wengi wapya kama wewe wameweza kukabiliana na mazingira na tayari wamezoea maisha ya jamii nchini Kanada.

Litakuwa ni jambo muhimu sana kwako kuzungumza Kiingereza au Kifaransa kwa maana itakusaidia kupata huduma, kutafuta kazi na kukupa uzoefu wa maisha nchini Kanada. Kama utakuwa na nafasi ya kujifunza lugha moja kati ya hizi kabla ya kuja Kanada, unapaswa uongeze ujuzi wako wa kutumia lugha. Baada ya kufika, unapaswa kutumia fursa zilizopo kuongeza ujuzi wa kuzungumza, kuandika na kusoma.

Waulize watu wanaokuzunguka maswali. Na ukiwa na mashaka, waeleze wadhamini wako

Kumbuka kuna watu na huduma ambazo ziko tayari kukusaidia.

**Taarifa hizi zimesasaishwa mwezi Aprili, mwaka 2014**